**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA WAZIRI MKUU**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (OWM - TAMISEMI)**
**HALMASHAURI YA MJI WA MBULU**

# SHULE YA SEKONDARI AYAMOHE


## NAMBA ZA SIMU:

**Mkuu wa Shule - +255 629 061 763**

**Makamu Mkuu wa Shule – 0782194799/0687146729**

**Shule ya Sekondari AYAMOHE**

**S. L. P 183, Mbulu Manyara - Tanzania**


Tarehe ………………

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi ………...................................................................**

**S.L.P ………………………………..................................................................**

Yah**:** <u>MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA **TANO** KATIKA SHULE YA SEKONDARI **AYAMOHE**, HALMASHAURI YA **MJI WA MBULU**, MKOA WA **MANYARA,** MWAKA……………..</u>

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka **……….** na atasoma tahasusi ya ………….

Shule ya Sekondari **AYAMOHE** ipo umbali wa **Kilometa 4.8** Mashariki mwa Mji wa **MBULU** Usafiri wa Daladala kutoka mjini **MBULU** unapatikana katika kituo cha mabasi **MBULU MJI** Nauli ni Shilingi **1,000 kwa Daladala** na **Pikipiki** ni Shilingi **2,000** .

Mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni **tarehe………………...** Mwisho wa kuripoti ni tarehe……………**.**

**2. Mambo muhimu ya kuzingatia:-**

**A. <u>Sare za Shule (Kwa wasichana)</u>**

i) Sketi rangi ya **MICKDOMA (ISTEM NAMBA MOJA RANGI NAMBA 1153) pea mbili**. Utajishonea, Rinda box kubwa nyuma na mbele. Urefu wa sentimita 30 kutoka kwenye magoti kuelekea chini
ii) Shati nyeupe yenye mikono mirefu pea mbili-Utajishonea / kujinunulia
iii) Tai ndefu yenye rangi ya **MICKDOMA**.
iv) Soksi jozi mbili nyeupe za shule;
v) Sweta 1 rangi ya chungwa iliyoiva (Golden yellow) ya shingo V.
vi) T-Shirt ataikuta shuleni ( Aje na shilingi elfu kumi na tano kwa ajili ya T-Shirt)

vii) **Kwa Waislam tu** waje na Suruali yenye rangi MICKDOMA (**ISTEM NAMBA MOJA RANGI NAMBA 1153**) pea mbili Utajishonea mwenyewe na isiwe ya mlegezo wala model

viii) Rangi ya **Hijab (kijuba) ni nyeupe** ifunike kifua cha mwanafunzi pia iwe ndefu kufikia kifundo cha mkono akisimama

ix) Sare za michezo:- Track suti rangi ya Kijivu, tisheti 1 ya kijani isiyo na maandishi yoyote, shingo duara na raba rangi nyeusi/nyeupe pea mbili

x) Viatu vya shule pea mbili ni vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi

xi) Tracksuit 1 ya rangi Nyeusi nzito yenye mistari nyeupe, Sweta Ienye kofia (Hoodies) ya rangi nyeusi na soksi ya kijivu nzito kwa ajili ya kuvaa usiku wakati wa kujisomea.

xii) Sketi 1 ya kazi rangi ya **URUJUANI** (**ISTEM NAMBA MOJA RANGI NAMBA 1120**) mshono marinda kwa ajili ya kazi za nje na t- shirt rangi ya Blue isiyo na maandishi yoyote shingo duara.

**B. <u>Sare za Shule (Kwa wavulana)</u>**

I. Suruali rangi ya **MICKDOMA (ISTEM NAMBA MOJA RANGI NAMBA 1153) pea mbili**. Zenye mifuko miwili ya pembeni na marinda mawili kila upande kwa mbele na upana wa chini wa suruali usipungue sm 16 (USISHONE MODO/MNYONYO)

II. Shati nyeupe yenye mikono mirefu pea mbili-Utajishonea / kujinunulia

III. Tai ndefu yenye rangi ya **MICKDOMA RANGI NAMBA 1153**

IV. Soksi jozi mbili kaki za shule;

V. Sweta 1 rangi ya chungwa iliyoiva (Golden yellow) ya shingo V.

VI. T-Shirt ataikuta shuleni ( Aje na shilingi elfu kumi na tano kwa ajili ya T- Shirt)

VII. Sare za michezo:- Track suti rangi ya Kijivu, tisheti 1 ya kijani isiyo na maandishi yoyote, shingo duara na raba rangi nyeusi/nyeupe pea mbili

VIII. Viatu vya shule pea mbili ni vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi

IX. Tracksuit 1 ya rangi Nyeusi nzito yenye mistari nyeupe, Sweta lenye kofia (Hoodies) ya rangi nyeusi na soksi ya kijivu nzito kwa ajili ya kuvaa usiku wakati wa kujisomea.

X. Suruali 1 ya kazi rangi ya **URUJUANI** (**ISTEM NAMBA MOJA RANGI NAMBA 1120**) Zenye mifuko miwili ya pembeni na marinda mawili kila upande kwa mbele na upana wa chini wa suruali usipungue sm 16 (USISHONE MODO/MNYONYO) kwa ajili ya kazi za nje na t- shirt rangi ya Blue isiyo na maandishi yoyote shingo duara.

**NB: PICHA ZA VITAMBAA VYA SARE ZA SHULE VIMEAMBATANISHWA UKURASA WA MWISHO WA MAELEKEZO YOTE. TAFADHALI PRINT UKURASA HUO KWA RANGI (COLOURED)**

**3. Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-**

i. Madaftari 10 (counter book Q4), kalamu za kutosha, Rula, mathematical set, Scientific calculator, **Ream Mbili (A4)** kwa mwaka na Dissecting kit kwa wanafunzi wa masomo ya Sayansi **PCB & CBG**.

ii. Mwanafunzi kwa TAHASUSI yake anashauriwa kujinunulia vitabu vya ziada na kiada kama ifuatavyo

1. PHYSICS – S.CHAND ONE, S.CHAND 2
2. ADVANCE MATHEMATICS – S.CHAND VOLUME 11 & 12, PURE 1 & PURE 2 (BACKHOUSE), MAYOMBIA 1&2
3. CHEMISTRY – NGAIZA SERIES- PHYSICAL CHEMISTRY, ORGANIC CHEMISRTY, GENERAL CHEMISTRY & INORGANIC CHEMISTRY
4. BIOLOGY – S.CHAND & BIOLOGICAL SCIENCE(BS)
5. ECONOMICS- ELEMENTARY ECONOMICS BOOK 5&6, ELEMENTARY ECONOMICS MGANDA, NA ECOMICS MSABILA FORM 5&6
6. KISWAHILI ONE – NADHARIA YA KISWAHILI (KRISTOPHA MWANSUKO)
7. KISWAHILI TWO – NADHARIA YA FASIHI SHULE ZA SEKONDARI KIDATO CHA 5&6 (2019) KILANGI ENOCK LUCAS, MSINGI WA FASIHI YA KISWAHILI NAZARIA YA KISWAHILI KIDATO CHA 5&6 KISWAHILI 2(2024) Godlove J Gwivaha
8. LANGUAGE – ADVANCE ENGLISH LEVEL A practical Approach by Nicolas Asheli, third edition. **NB: (Kwa ushauri wa vitabu hapo juu wasiliana na namba ya simu – 0629 061763)**

iii. Barua ya maagizo (Joining instruction)

iv. Vyeti vyako (Vivuli vya vyeti) vya kidato cha nne (IV) Academic, Leaving na cheti cha kuzaliwa.

v. Cheti cha daktari (medical Examination Certificate) ambacho kimejazwa

vizuri na Mganga mkuu wa hospitali ya Serikali

vi. Fomu ya makubaliano ya mzazi kumsomesha mwanae (Fomu zimeambatanishwa nyuma ya barua hii)
vii. Mto mmoja na foronya 2 za rangi ya blue bahari.
viii. Mashuka Jozi 2 rangi ya PINK kwa wasichana na LIGHT BLUE kwa wavulana, blanket 1 nzito, chandarua 1 ya Duara rangi ya blue, Taulo (1) & Nightdress (Tracksuit nyepesi ya kulalia kwa wavulana, Gauni refu ya kulalia kwa wasichana)
ix. Mwavuli 1, buti ya matope (Rain boots) Fupi Rangi Nyeusi kwa ajili ya shughuli za nje wakati wa mvua
x. Aje na Godoro inch 3 kwa futi $2^1/2$
xi. Vyombo vya chakula: - Sahani ya bati, (Aluminium) kikombe, bakuli na kijiko.
xii. Sanduku la bati/chuma la kufunga kwa kufuli imara kwa ajili ya kuhifadhi vifaa vyako.

xiii. Mwanafunzi aje na BIMA ya Afya kwa ajili ya matibabu yake.
xiv. Ndoo tatu (3) yenye ujazo wa lita 10 zenye mifuniko kwa matumizi yake binafsi
xv. Jembe 1 lenye mpini imara, Brashi ndogo ya chooni 1 na mopa moja kwa ajili ya kazi za shule. (**Kwa wanafunzi wa Tahasusi ya HKL NA PCB**)
xvi. Mopa 1, kwanja/fyekeo 1, na hard broom 1 kwa ajili ya kufanyia usafi.( **Kwa wanafunzi wa Tahasusi ya PCM** na **EGM**)
xvii. Jembe 1 lenye mpini imara, soft broom ya duara 1 na mopa moja **(Kwa wanafunzi wa Tahasusi ya CBG na PGM)**
xviii. Nguo za ndani za kutosha

**MUHIMU:** ***Ili kumpunguzia Mzazi/Mlezi gharama za kusafiri na mizigo mingi, shule inapenda kukujulisha kuwa vifaa vingi anavyotakiwa kuja navyo mwanafunzi kama vile Ream, jembe, ndoo, Fyekeo, mopa, fagio, Brashi ndogo ya usafi wa chooni n.k vinapatikana MBULU MJINI.***

**4. Michango mbalimbali**

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 2. | Tahadhari | 5,000/= |
| 3. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| 4. | Nembo ya Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

NB: Fedha zilipwe Benki kwa **Ac.No. 41210024225** Bank ya **NMB**. Jina la AKAUNTI. **AYAMOHE SEKONDARI AKAUNTI YA WAZAZI.** Fedha za matibabu zitapokelewa shuleni kama mwanafunzi hana Bima ya Afya watapatiwa Bima ya pamoja shuleni kwa TSH 50,400 TU. Wenye kadi ya Bima ya Afya waje nazo shuleni.

Utakapofika shuleni unatakiwa kuwasilisha **"bank pay-in slip**" iliyoandikwa jina kamili la mwanafunzi kwa mhasibu wa shule ili akuandikie stakabadhi ya malipo.

**5. Sheria na Kanuni muhimu za Shule**

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha,

inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

## 6. Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku( Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.
xii. Mwanafunzi haruhusiwi kusuka nywele.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**

- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi**

**kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**

- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

**7. Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Kusuka nywele.
vii. Kufuga ndevu;
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ix. Uvutaji wa sigara;
x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xii. Kusababisha mimba;
xiii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiv. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xvi. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu.
xviii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**8. Viambatisho na Fomu Muhimu**

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai
iii. Fomu ya Mzazi ya kukiri mwanafunzi atafuata sheria na kanuni za shule

**FOMU YA UCHUNGUZI WA AFYA (MEDICAL EXAMINATION FORM) AMBAYO ITAJAZWA NA MGANGA MKUU WA HOSPITALI YA SERIKALI**

Mimi (Jina la Mganga Mkuu wa Wilaya)

… ..................................................................................................... Ninathibitisha kuwa mwanafunzi huyu (Jina la mwanafunzi)........................................................................... Amepimwa nami kikamilifu na kuonekana kuwa anayo/hana afya nzuri kwa mujibu wa taarifa zifuatazo:-

(a) HALI YA MWILI:-

(i) Mapigo ya moyo ……………………………………………………………

(ii) Haemoglobin (HB) …………………………………………………………

(iii) Kundi la damu (blood group) …………………………………………….

(iv) Mkojo (Urine) …………………………………………………………..

(v) Kinyesi (stool) …………………………………………………………..

(vi) Macho (Eye) ……………………………………………………………

(vii) Masikio (Ear)……………………………………………………………

Angalia:- Weka maoni yako kuhusu kila kilichotajwa (a) (i) – (vii)

(b) MAGONJWA:-

*Amewahi/hajawahi/ana/hana/magonjwa yafuatayo:-

(a) Pumu ………………………………………………………………………………

(b) Kifua kikuu …………………………………………………………………..

(c) Kifafa ………………………………………………………………………………

(d) Shinikizo la damu chini/juu ………………………………………………………..

(e) Vidonda vya tumbo ………………………………………………………………

(f) Maradhi ya zinaa ………………………………………………………………….

(g) Ukoma …………………………………………………………………………….

(h) Mental illness (ugonjwa wa akili ) …………………………………………………

(i) Maradhi mengine yasiyotajwa hapo juu:-

…………………………………………………………………………………………

SAHIHI NA MHURI WA DAKTARI /MGANGA

TAREHE ……………………………

## FOMU YA KUKIRI KUKUBALIANA NA SHERIA, KANUNI NA MAELEKEZO MENGINE YANAYOTOLEWA NA SHULE

**SEHEMU A (Ijazwe na mwanafunzi)**

1. Jina la mwanafunzi (majina matatu) ………………………………………..
2. Uraia………………………………………………………  ……………………
3. Tarehe ya kuzaliwa……………………………………………………………
4. Shule anayotoka …………………………………………………..................
5. Tarehe ya kutoka shule hiyo ……………………………………………...

**SEHEMU B.** (Ijazwe na mzazi / mlezi)

1. Jina la mzazi / mlezi (majina matatu) ………………………………………..
2. Anwani ya mzazi/mlezi ………………………………………………………
3. Mahali anapoishi ……………………………………………………………..
4. Mawasiliano ya Mzazi/Mlezi(namba ya simu)…………………………………
5. Kazi ya mzazi/ mlezi …………………………………………………………

Mahali anapofanya kazi ……………………………………………………..

6. Ndugu wawili wa karibu (wanaweza kuwa badala ya mzazi)

NB:Mwanafunzi atatembelewa Jumamosi ya mwisho wa mwezi

Jina la Ndugu wa I…………………………………..…Namba ya Simu…………

Anuani yake: ………………………………………..…Uhusiano………………

Jina la Ndugu wa II: ………………..……………Namba ya Simu………………

Anuani yake ……………………………..…Uhusiano wake : …………………….

Tarehe:………………………… Sahihi ya Mzazi:………………………

**FOMU YA MZAZI / MLEZI KUKUBALI WAJIBU WA KUMSOMESHA MWANAFUNZI**

Mimi ………………………………………… wa kijiji cha …………………… ….

Kata ya ………………………………Halmashauri ya……………………………

Ambaye ni mzazi/mlezi wa ……………………………………..……………..

Anayeingia kidato cha .................................................katika shule ya sekondari Ayamohe najifungia wajibu huu kwa ajili ya kumsomesha mwanafunzi tajwa hapo juu mbele ya utawala wa kijiji changu hiki. Nimesoma barua ya kumwita shuleni, sheria za shule na fomu zote zilizoambatishwa, nimeelewa kila kitu na kuridhika. Pia najua nisipotimiza masharti yote mwanafunzi huyu hatopokelewa shuleni. Nakubali ahadi hiyo nikijua ni ahadi ambayo sitaweza kuikiuka bila hatua za kisheria zinazostahili kuchukuliwa dhidi yangu.

Sahihi ya mzazi au mlezi …………………………….. Tarehe ………………..


sahihi ya afisa mtendaji …………….Tarehe …………Namba ya simu………

# PICHA ZA VITAMBAA VYA SARE ZA SHULE
## TAFADHALI PRINT UKURASA HUU KWA RANGI (COLOURED)

## WAVULANA



Shati nyeupe, mikono mirefu



Kitambaa cha suruali ya shule



Sweta la Shule



Kitambaa cha Suruali ya kushindia




Sweta Jeusi (Hoodie) lenye kofia na mikono mirefu

## WASICHANA




Shati nyeupe, mikono mirefu



Kitambaa cha Sketi ya shule



Sweta la Shule



Kitambaa cha Sketi ya kushindia



Sweta Jeusi (Hoodie) lenye kofia na mikono mirefu